## Maswali

1. Mbona Mungu alituma tauni kwa nchi ya Misri?
2. Tauni ya kwanza ilikua nini?
3. Tauni ya pili ilikua nini?
4. Farao alifanya nini kila mara Mungu aliondoa tauni?
5. Tauni zote zilikuja kwa Waisraeli?
6. Tauni ya mwisho yenye Mungu alitumia Wamisri ilikuwa gani?
7. Mungu aliambia Waisraeli wafanye nini?
8. Nini ilifanyika kwa Wamisri saa za usiku wa manane?
9. Nini ilifanyika kwa Waisraeli?
10. Farao aliambia Musa na Haruni wafanye nini baada ya tauni ya mwisho?

## Majibu

1. Kwa sababu Farao alikataa kuruhusu Waisraeli waende.
2. Tauni ya kwanza ilikua maji kugeuka kuwa damu.
3. Tauni ya pili ilikua ya vyura.
4. Farao alibadilisha mawazo yake na kukataa kuruhusu Waisraeli waende.
5. Tauni za kwanza 3 ndio zilikuja kwa Waisraeli Gosheni.
6. Tauni ya mwisho ilikuwa kua wana wazaliwa wa kwanza.
7. Ua mwana kondoo, paka damu yake kwa kuzungusha mlango, oka hiyo nyama na wakule pamoja na mkate usiotiwa chachu na mboga zenye uchungu.
8. Malaika wa kifo alitembea Misri yote akiua wana wazaliwa wa kwanza wote.
9. Malaika wa kifo aliruka nyumba za Waisraeli zote zenye zilikuwa zimepakwa damu kwa mlango.
10. Farao aliambia Musa na Haruni watoe Waisraeli Misri.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 18 Musa na tauni kumi

**Kwa Biblia** Kutoka mlango wa 7:14 mpaka mlango wa 12:31

### Kiini cha somo

Kuonyesha hukumu ya Mungu inayo okogofya kwa watu waovu. Lakini Mungu ni mwema na analinda watu wake.

### Somo

Farao hakuwaacha Waisraeli warudi kwa nchi ya Kanaani. Mungu alimwambia Musa kwamba ataleta tauni za kumteza Farao. Musa na Haruni walimwambia Farao, “Mungu anasema, ‘kama hautaacha watu wangu waende nitageuza maji ya Misri yote kuwa damu.’” Farao alijibu, “La sitawaacha waende.” Kwa hivyo Haruni alinyosha fimbo kwa Mto wa Nile. Maji yote yaligeuka kuwa damu. Kwa siku saba hakukuwa na maji katika nchi ya Misri; yote ilikuwa damu. Samaki kwa mito walikufa. Kulikuwa na harufu mbaya.

Baada ya siku saba Musa akamwambia Farao, “Mungu anasema, ‘Usiporuhusu watu wangu waende, nitajaza nchi na vyura.”’ Farao alijibu, “La sitawaruhusu waende!” Haruni alinyosha fimbo juu ya mito na vijito. Maelfu ya vyura waliruka nje. Walifunika nchi ya Misri. Kulikuwa na vyura kila mahali, nyumba zilijaa vyura, walikuwa kwenye vitanda, walikuwa kwa tanuu ndani ya chakula, chini kwa miguu ya kila mtu.

Halafu Farao akaita Musa na Haruni. Walikubali na kumwambia Farao kwamba Mungu ataondoa vyura ikiwa ataruhusu Waisraeli waende. Siku ifwatayo Mungu aliua vyura vyote. Watu walisanya zote pamoja. Lakini nchi yote ilikua na uvundo.

Baada ya vyura kuisha, Farao alibadilisha mawazo yake. Alikataa kuwaruhusu Waisraeli kuenda. Kwa hivyo Mungu akatuma tauni ya chawa. Watu wote walifunikwa na chawa. Halafu Farao akaita Musa na Haruni. Farao alikubali Waisraeli waende ikiwa Mungu atatoa chawa.



Siku ifwatayo chawa zilikuwa zimeisha. Lakini Farao alibadilisha mawazo yake tena. Hakuruhusu Waisraeli waende. Kwa hivyo Mungu akatuma tauni ya mainzi kwa nchi ya Misri. Lakini hakukua na mainzi katika Gosheni kwenye Waisraeli waliishi. Hakukua na tauni tena Gosheni. Mungu alikuwa anaonyesha Farao na Wamisri nzima kwamba tauni zilikuwa adhabu. Mungu alituma tauni kwa sababu Farao hakumtii. Ilionyesha Waisraeli kwamba Mungu alikuwa anatumia uwezo wake kuwasaidia.



Muda si muda Farao akaita Musa na Haruni. Alikubali kuwaruhusu Waisraeli waende ikiwa wataondoa mainzi. Lakini bude tu mainzi zilipokwisha, Farao alibadilisha mawazo yake. Hakuruhusu Waisraeli waende.

Tena Mungu alituma tauni iliyouwa n'gombe wote. Tena Mungu alituma tauni ya majipu. Kila mtu alifunikwa na majipu. Hawakuweza kukaa chini wala kulala kwa sababu majipu yalikuwa ya vidonda pia. Tena Mungu akatuma tauni ya mvua ya mawe. Hayo mawe yalikuwa kubwa mpaka yakaua wanyama wote na kuharibu mimea yote. Baada ya hiyo, Mungu alituma tauni ya nzige. Kundi kubwa la nzige lilifunika nchi. Nzige walikula majani na mimea yote katika nchi ya Misri. Baadaye Mungu alituma tauni ya giza. Giza kilikuwa kingi mpaka kila mtu alikaa nyumbani kwa siku tatu.



Farao aliendelea kubadilisha mawazo yake. Kila mara Mungu alipotuma tauni, Farao alisema Waisraeli wangeenda. Lakini baada ya Mungu kutoa tauni, Farao alibadilisha mawazo yake. Hakuwaruhusu Waisraeli waende.

Mungu aliambia Musa kwamba atatuma Misri tauni moja ya mwisho. Wana wote wazaliwa wa kwanza wa Wamisri watakufa. Wana wa Waisraeli watapona ikiwa watatii maagizo ya Mungu.

Musa aliambia Waisraeli lazima wafanye vile Mungu amesema. Siku ya 14 ya mwezi kila familia ya Waisraeli lazima iuwe mwana kondoo. Lazima kunyunyiza damu ya mwana kondoo kwa miimo ya mlango ya nyumba zao na juu ya vizingiti wakitumia mmea wa hisopu. Lazima nyama iokwe jioni na waile pamoja na mboga zenye uchungu na mkate usiotiwa chachu. Lazima wale hicho chakula kama wamevaa na vitu vyao vimewekwa tayari kusafiri.

Waisraeli walifanya kila kitu vile Mungu alikua amewambia kufanya. Walikula chakula jioni. Ilipofika usiku wa manane Mungu alituma malaika kuua wana wazaliwa wa kwanza wa Wamisri. Waisraeli walikuwa wamezungusha damu ya mwana kondoo kwa milango yao. Malaika alipoona damu kwa mlango, aliruka hiyo nyumba. Hakuua mtu yeyote hapo. Waisraeli wanakiita hicho chakula 'Pasaka' kwa sababu malaika wa kifo alipita juu ya nyumba zao. Mungu aliamrisha Waisraeli wawe na siku kuu ya Pasaka kwa hiyo tarehe kila mwaka. Wanaiweka hiyo siku kuu kwa kukumbuka vile Mungu aliwaokoa kutoka Misri.

Malaika aliua kila mzaliwa wa kwanza Misri. Aliua mwana wa Farao na mwana wa mjakazi wa chini kabisa. Kila familia ya Misri ililia mwana wao. Lakini wana wa Waisraeli walipona

Mwishowe Farao aliona ni lazima atii Mungu. La sivyo Wamisri watakufa wote wasipowaacha Waisraeli waende. Farao aliita Musa na Haruni waje. Aliwambia kwamba Waisraeli waondoke Misri mara moja. Wamisri walipea Waisraeli dhahabu, fedha na vitu vingine vya dhamana na kuwambia waondoke Misri haraka.

Usiku huo Waisraeli mia sita elfu pamoja na watoto wao walitoka Misri. Ilikuwa ni mara ya kwanza watu kusafiri kwa nambari kubwa hivyo. Waisraeli walikuwa wamefunga misigo yao zamani. Walikuwa wamevaa na wako tayari kusafiri. Waliondoka Misri haraka - kabla Farao hajabadilishe mawaza yake.